# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

**HOTUBA YA**

**DKT. SALIM AHMED SALIM**

**YA KUKUBALI UTEUZI NA KUSIMIKWA KWAKWE KUWA**

**MKUU WA CHUO KIKUU CHA KUMBUKUMBU YA HUBERT KAIRUKI**

JUMAMOSI, NOVEMBA 01, 2003
UKUMBI WA KARIMJEE
DAR ES SALAAM

**HOTUBA YA DKT. SALIM AHMED SALIM YA KUKUBALI UTEUZI NA KUSIMIKWA KWAKE KUWA MKUU WA CHUO KIKUU CHA KUMBUKUMBU YA HUBERT KAIRUKI JUMAMOSI NOVEMBA 01, 2003 KATIKA UKUMBI WA KARIMJEE, DAR ES SALAAM**

Ndugu Mgeni Rasmi,
Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Dkt. Ali Mohamed Shein,
Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu,
Dr. Pius Ngw'andu,
Mheshimiwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, Bibi Kokushubila Kairuki,
Mheshimiwa, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Prof. F. J. Kaijage,
Mheshimiwa, Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Esther Mwaikambo,
Waheshimiwa Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu mbalimbali mliopo hapa,
Waheshimiwa Mabalozi,
Waheshimiwa Waalikwa wote,
(Itifaki imezingatiwa)

Awali ya yote nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Chuo kwa heshima hii kubwa niliyopewa kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki.

Mwezi Januari, 2001, Mkuu wa Chuo mwanzilishi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, marehemu Dkt. Omar Ali Juma, alifanya ziara ya uzinduzi chuoni. Wakati huo, ilikuwa imetimia miaka miwili tangu mwanzilishi na Makamu wa Mkuu wa Chuo wa Kwanza, marehemu Hubert Kairuki alipofariki. Mwezi Januari 2002, nilipata fursa ya kufanya ziara ya uzinduzi chuoni, baada ya kuombwa na Bodi ya Wadhamini ya Chuo kuwa Mkuu wa Chuo wa Pili kujaza nafasi iliyoachwa wazi na marehemu Dkt. Omar Ali Juma.

Kusema kweli, ilinibidi kufikiria sana kabla ya kukubali ombi la Bodi ya Wadhamini la kuwa Mkuu wa Chuo wa Pili wa Chuo Kikuu hiki. Kusita kwangu kwa mwanzo, hakuhusiani na tathmini yangu kuhusu umuhimu na faida za asasi hii ya elimu ya juu, kwa kuwa umuhimu huu ni jambo pla dhahiri. Bali, ni kutokana na mimi mwenyewe kuitambua mipaka yangu na nilitaka kujihakikishia mwenyewe kama nitaweza kuwa wa msaada kwa Chuo Kikuu hiki.

Lakini wasiwasi wowote ule niliokuwa nao, uliondolewa na mambo makuu wawili ya msingi. Kwanza, nimetiwa moyo na dira na kujitoa kwa dhati kwa Mkuu wa Chuo mwanzilishi, ambaye pamoja na majukumu yake mengi ya kitaifa, alikubali kuwa Mkuu wa Chuo. Vilevile, nilivutiwa sana na dira pamoja na michango ya Mwanzilishi na Makamu wa Mkuu wa Chuo. Watanzania hawa wawili maarufu waliotutoka, Marehemu Dkt. Omar Ali Juma na Marehemu Profesa Hubert Kairuki, wameweka mfano kwa jinsi walivyoupa umuhimu maendeleo na uendelezaji wa elimu ya juu katika jamii yetu.

Jambo la pili ni imani yangu juu ya umuhimu mkubwa wa kuhimiza maendeleo ya raslimali-watu ndani ya nchi yetu na katika bara letu la Afrika. Hapana shaka wala ubishi kuwa huu ndio ufunguo wa maendeleo ya kila nchi. Ni dhahiri pia kwamba jambo hili ni muhimu zaidi kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania.

Nilipata fursa ya kukitembelea Chuo na kujionea mwenyewe vitivo vyake mbalimbali na maeneo mbalimbali ya shughuli zake. Ziara hiyo ilinipa mwanga mkubwa kuhusu jinsi mambo yalivyo, mafanikio yaliyofikiwa na changamoto nzito ambazo bado ziko mbele yetu. Ziara yangu na mazungumzo tuliyoyafanya yalifafanua kwa uwazi zaidi mambo makubwa yaliyo mbele yetu na yatakayopatikana kwa kuzingatia dira ya waanzilishi wa Chuo Kikuu hiki.

Naamini kwamba wale wote ambao tunahusika na Chuo hiki tutatenda kazi zetu kwa kuzingatia dira hiyo.

Niruhusuni, kurudia shukrani zangu kwa heshima mliyonipa kuwa Mkuu wa Chuo hiki kichanga na chenye kuonyesha matumaini makubwa. Nawaomba wale wote waliohusika katika kufanya uamuzi huu, kupokea shukrani zangu na ahadi yangu kuwa nitajitahidi kufanya kila linalowezekana kuzikabili changamoto zinazoandamana na jukumu hili. Mimi kwa upande wangu, nitajitahidi sio tu katika kutia mwega juhudi zenu, bali pia kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya asasi hii. Hii ndio maana nakubali kwa moyo mkunjufu kuwa Mkuu wa Chuo wa Pili, na ni jambo la faraja kwangu kuongoza mahafali haya ya kwanza. Napenda kuwapongeza wale wote waliofanya kazi bila kuchoka na kutuleta pamoja leo hii. Napenda kutoa pongezi za dhati kwa wahitimu kwa kuwa waanzilishi.

Serikali yetu imetamka mara kwa mara sera yake ya kusaidia shirika lolote lile ambalo limeonyesha nia ya kuchangia katika maendeleo ya taifa. Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki na shirika lake dada, Hospitali ya Mikocheni, kwa hakika yamo ndani ya kundi hilo lenye nia njema. Nina imani kuwa Serikali itaangalia ni kwa jinsi gani itasaidia jitihada za asasi hizi. Kushiriki kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Mohamed Ali Shein kwa niaba ya Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ni kielelezo tosha ya jinsi Serikali yetu inavyothamini juhudi kama hizi. Nachukua fursa hii kutoa shukurani zetu kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais na kupitia kwake kwa Mheshimiwa Rais na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kimsingi, Chuo Kikuu kinatakiwa wakati wote kulenga shughuli zake katika Ufundishaji, Utafiti, Huduma na Ushauri kwa kushirikiana na washirika wa ndani na nje katika sekta ya umma na binafsi. Chuo chetu hiki cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, kama kimojawapo cha Vyuo Vikuu, kinapaswa kuzingatia malengo hayo kwa kuwa na washirika wengi ndani na nje ya nchi

yetu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba washirika wetu katika maendeleo, wa nchini na nje ya nchi, kusaidia asasi binafsi kama hizi ambazo zitaisaidia Tanzania kutoa huduma nzuri kwa watu wake. Hapa, ningependa kulishukuru Shirika la Ford Foundation kwa msaada wake katika utekelezaji wa mpango wa kimkakati. Naamini kwamba Mtandao wa Mikocheni wa "**Afya na Elimu**" ni mfano mzuri wa jinsi asasi binafsi zinavyoweza kusaidia katika maendeleo ya taifa.

Nawatakia mafanikio mema.

Nawashukuru kwa kunisikiliza.